

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

Mkoa : Kilimanjaro  
Simu : 27- 2758441  
Fax : 27- 2756102



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
S.L.P. 27,  
HAI.

[mkurugenzihai@yahoo.co.uk](mailto:mkurugenzihai@yahoo.co.uk)  
[www.haidc.go.tz](http://www.haidc.go.tz)

Kumb.Na.LG/B.20/7

Tarehe: 14/07/2017

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA**

Halmashauri ya Wilaya ya Hai imepokea kibali cha ajira mpya cha Wasaidizi wa Hesabu katika vituo vya Afya chenye Kumb. Na.FA.79/85/01"E"/04 cha tarehe 06/07/2017. Kutokana na kibali hicho; Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza **nafasi nne (4)** za kazi ya **Wasaidizi wa Hesabu**.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au Sita.
2. Awe amehitimu mafunzo ya cheti cha ATEC level II au "Foundation Level" kinachotolewa na NBAA au vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

**B. MAJUKUMU YA KAZI**

1. Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za uhasibu.
2. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha.
3. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu.
4. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki.
5. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana.

**C. MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B sawa na Tsh. 390,000/= kwa mwezi.

**D. MASHARITI YA KAZI:**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 hadi 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Nafasi ya kazi inayoombwa iandikwe katika kichwa cha habari cha barua kutozingatiwa hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma na Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.  
**"Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 28 Julai, 2017 saa 9.30 Alasiri.
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Hai,  
S.L.P.27  
HAI.

AU

District Executive Director,  
Hai District Council,  
P.O. Box 27,  
HAI



.....  
**YOHANA E. SINTOO**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**